Toleo 54

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## MIFANO NA VIVULI: KRISTO NDIYE KILE KILICHO HALISI

Kutoka mwanzo Mungu alipanga ibada za wana wa Israeli, sadaka zao, pamoja na taratibu zao kwa kusudi la kiungu. Hizi hazikuwa sherehe ambazo hazikuwa na mpangilio, bali zilikuwa ishara za michoro iliyoashiria jambo kuu zaidi la kweli.

Katika Agano la Kale Maandiko yanasema kuhusu aina fulani ya sherehe, matukio, na watu fulani, kwamba haya yote yalikuwa ni vivuli, michoro, pamoja na "aina" ambazo zilimwangazia Kristo, kabla ya Yeye kufika hapa duniani: haya yote yanajulikana kama "mifano." Hivi vilikuwa ni vivuli vya awali, vilivyoashiria ukweli halisi wa kiroho unaopatikana katika Agano Jipya. Waebrania 10:1 inatangaza kwamba, "Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao." Mtume Paulo naye ameeleza katika Wakolosai 2:17 kwamba mambo haya yalikuwa "ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo."

Vivuli hivi havikutolewa na Mungu ili kuwakanganya watu, bali vilikuwa ni kwa ajili ya kuwafunza. Katika kila matoleo, tambiko, na mahali patakatifu, Mungu alikuwa akiwafundisha watu wake masomo kuhusu utakatifu, sadaka, na njia ya mtu kuweza kufika kwake. Sadaka zilizotolewa mara kwa mara, utakatifu wa makuhani, na kutengwa kwa Mahali Patakatifu, yote yalikuwa mambo yalioashiria ukamilifu ambao ungepatikana tu ndani yake Kristo. Mpangilie huo wote ulikuwa kama mwalimu wa shule aliye na kazi ya kuwandaa watu kwa ajili ya Masihi.

Katika Agano la Kale, mifano hii ilikuwa ni vivuli, ilhali ukamilifu wake sambamba unapatikana katika Agano Jipya—ambako kunapatikana kile kilicho halisi. Kile ambacho mbeleni kilionekana kwa mwili na kinachopatikana katika historia ya nyakati za Sheria, kilipata ukamilifu wake wa kweli katika Kristo, likiwa ni jambo la kiroho lenye uhalisi wa milele. Kupitia michoro na aina hizi zilizopeanwa na Mungu, njia ya wokovu ilipewa mifano yake ya awali, ili kwamba Kristo atakapokuja watu wake waweze kumtambua kama mwokozi aliyeahidiwa.

Biblia yenyewe inatupatia mifano dhahiri. Adamu, mwanadamu wa kwanza alikuwa "mfano wake yeye atakayekuja" (Warumi 5:14). Huyu Adamu alikuwa ni mfano wa Kristo, "Adamu wa mwisho," ambaye alileta uhai; ilhali Adamu wa kwanza alileta kifo. Adamu alijisalimu kwa majaribu yaliyomkumba, na kwa njia hiyo akawaletea wanadamu dhambi; lakini Kristo alishinda na kutuletea haki na tumaini.

Mwanakondoo wa Pasaka ni mfano mwingine ambao unajulikana sana. Damu ya mwanakondoo ambayo ilipakwa milangoni mwa nyumba huko Misri iliwaokoa wana wa Israel dhidi ya mwangamizi. Katika Agano Jipya, Yesu Kristo anadhihirishwa kama Pasaka yetu, ambaye ametolewa sadaka kwa ajili yetu (1 Wakorintho 5:7). Mwanakondoo alikuwa ni kivuli; Kristo ndiye halisi na damu yake inatukomboa kutokana na kifo na mauti.

Nyoka wa shaba ambaye aliinuliwa huko jangwani ni mfano mwingine. Wakati wana wa Israeli walipoumwa na nyoka, walipata uponyaji kwa kumtazama nyoka huyo. Naye



"Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa." (Yohana 3:14).


| Mifano na Vivuli | Tahariri | Maskani ya Mungu | Mapambo za Maskani | Sanduku la Agano |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 3 | 4-5 | 6-7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

Yesu akasema, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa" (Yohana 3:14). Kama vile wana wa Israeli walimtazama nyoka huyo kwa imani, ndivyo tunahitaji kumtazama Kristo kwa ajili ya uzima wetu wa milele.

Hata ile Maskani ya Mungu, pamoja na mapambo na huduma zake, ni aina nyingine za mifano. Waebrania 8:5 inatwambia kwamba hii ilitumika kama "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni." Kwa kila maelezo yake, kuanzia kwa Madhabahu ya Sadaka za Kuchomwa, hadi pale Patakatifu pa Patakatifu, yote hayo yalimwashiria Kristo pamoja na mpango wake wa wokovu. Hii yote ilionyesha kwamba njia ya kufikia uwepo wake Mungu haikuwa imefunguka; lakini katika Kristo pazia ikapasuka na tukawezeshwa kumfikia Baba.

Ukuhani wenyewe ulikuwa mfano mwingine, ambao uliashiria huduma ya milele ya Kristo. Kuhani mkuu, ambaye aliingia pale Patakatifu pa Patakatifu mara moja kwa mwaka, alikuwa kivuli cha awali cha Yesu, ambaye ni Kuhani Wetu Mkuu, "kwa mfano wa Melkizedeki" (Waebrania 6:20). Yeye ambaye alijitoa mara moja kwa ajili ya watu wote, na daima anaishi ili kutuombea. Vivyo hivyo, wakati wana wa Israeli walipokunywa maji huko jangwani kutoka kwa mwamba, mtume Paulo anasema kwamba "Mwamba ule ulikuwa ni Kristo" (1 Wakorintho 10:4). Kama vile maji hayo yalidumisha maisha yao ya kimwili, ndivyo Kristo anavyowapatia maji ya uzima wa Roho wote ambao wanamwamini.



Mfumo wa Agano la Kale ulikuwa wa muda, na haungeweza kufanya waliotumika chini yake kuwa wakamilifu. Lakini kivuli hiki kiliandaa njia kwa kile ambacho ni halisi kabisa—yaani Kristo Mwenyewe. Historia ya Israeli ilifundisha masomo yafuatayo: Misri ilikuwa ni mchoro wa utumwa wa dhambi, Musa naye alikuwa ni mfano wa Mkombozi aliye Kristo; nayo nchi ya Kanaani ilikuwa kivuli cha awali cha urithi na ushindi wa maisha yaliyojazwa Roho Mtakatifu. Waebrania 9:11 inatangaza kwamba: "Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu." Vivuli hivi sasa vimeondoka na mahali pale kuchukuliwa na kile ambacho ni kamili kabisa na kinachodumu; vidokezi sasa vimeondoka, na sasa tuna uhalisi wa mambo.

Mifano hii inadhihirisha umoja wa Maandiko na hekima ya mpango wa Mungu. Agano la Kale na Agano Jipya sio hadithi mbili tofauti, bali ni ufunuo wa kiungu ambao ulidhihirishwa tangu mwanzo hadi mwisho. Kile ambacho Mungu alipatia Israeli kama michoro, sasa kimedhihirishwa kwa ukamilifu wake kupitia Yesu Kristo. Kwa kujifunza kuhusu mifano na vivuli hivi, tunaona jinsi Mungu aliandaa njia ya wokovu kwa umakini mkubwa, na jinsi ahadi zake zinatimizwa ndani ya Mwanawe kwa njia iliyo na urembo mkuu. Kile ambacho wakati mmoja kilifichwa katika aina na sherehe tofauti, sasa kimedhihirishwa katika Injili.

Kujifunza kuhusu mifano hii kunatupatia uhakika kwamba uandishi wa Maandiko ulikuwa ni jambo la kiungu. Vivuli hivi vilikuwa vya muda; lakini kile kilicho halisi ni cha milele. Ndani yake Kristo kila mfano umekamilika—Yeye ndiye Mwanakondoo wa kweli, Kuhani Mkuu wa Milele, na Hema la Makutano ambalo liko hai. Kupitia kwake tunaweza kumfikia Mungu, tunapata msamaha wa dhambi, na pia Roho wake Mtakatifu anadumu ndani yetu. Yeye ndiye kile kilicho halisi na chenye utukufu, kile ambacho mbeleni kilinongonezewa kupitia vivuli, sasa kiko dhahiri ndani yake Kristo.

# Tahariri



*Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa.* —Waebrania 10:1

Mpango wa wokovu ulio na utukufu mwingi kupitia Yesu Kristo ulipewa kivuli chake cha awali kwa ibada za watu wa Mungu, ambao walikuwa chini ya Sheria ya Musa. Agano la Kale ni mfano wenye urembo wa ujuzi wa ajabu ambao sasa umepata ukamilifu wake katika Agano Jipya.

Katika robo hii ya mwaka tunajifunza kuhusu mifano na vivuli, hasa vile vya Maskani ya Mungu na mapambo zake. Ishara ambazo zinapatikana katika Maskani ya Mungu hazikuweko kwa bahati tu, bali zilizinduliwa na Mungu ili kudhihirisha urembo wa mpango huo mkuu wa kiungu.

Mifano ambayo inadhihirishwa kupitia sadaka za wanyama ambazo zilitolewa kwa ajili ya dhambi, uogaji katika Birika la Shaba, kuchomwa kwa ubani katika Madhabahu ya Dhahabu, yote hayo ni mambo ambayo yanakusudiwa kuleta mwangaza. Nao ushirika uliofanyika kati ya mwanadamu na Mungu hapo katika Kiti cha Rehema ni jambo ambalo linaleta mshangao mkuu na kuzua heshima kwa Mungu ndani yetu. Maelezo ya mifano inayozungumziwa kwenye gazeti hili yanatokana na Maandiko, na kusudi lake ni kuangazia kazi ya ukombozi wa Kristo. Lakini hata ingawa maelezo mengi ya Maskani hayo yaliashiria kweli fulani za kiroho kwa njia iliyokuwa wazi, sio kila maelezo ya Maskani hayo yanatakiwa kuchukuliwa kuwa ni ishara iliyo na maana zaidi ya jinsi ambavyo inaelezwa katika Biblia. Basi tunawahimiza wasomaji wetu kuwa waangalifu wanaposhughulikia swala hili la mifano, daima wakihakikisha kwamba Kristo ndiye aliye halisi na wa kweli katika kila jambo.

Kama mimi ningekuwa mwandishi wa nyimbo, ningeandika kuhusu mshangao na uvuvio ambao unazuka moyoni mwangu kutokana na masomo na ukweli wa ujuzi tulio nao katika Agano Jipya. Tunapojifunza mambo haya yote kwa msingi wa mifano na vivuli, kweli za mpango wa ukombozi wa Mungu zinakuwa dhahiri zaidi hata katika siku hizi zetu.

Hebu basi na tumshukuru Mungu kwamba leo tuna mambo bora zaidi kushinda yale wana wa Israeli walikuwa nayo katika Maskani yake Mungu. Je, wewe msomaji ungali umesimama katika Ua la Maskani hayo au tayari umeingia mahali Patakatifu pa Patakatifu? Mlango uko wazi kwa damu ya Yesu, hebu basi ingia ndani!

Michael W. Smith

Oktoba, 2025

*Tutembelee*

*www.thegospeltruth.org*

*ili kujiandikisha na*

*kupata jarida*

*za mbele.*




**"Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani."**

**Wagalatia 3:24**

# Maskani ya Mungu

## Mifano na Ukamilifu Wake

Mungu hangedumu katika mioyo ya watu ambao hawakuwa watakatifu, ndiposa akampatia Musa mchoro wa kufuata wakati wa kujenga Maskani yake, na kutoka ndani ya Maskani hayo ndiko Mungu alidumu kati ya watu wake (Kutoka 25:8-9). Maskani ya Mungu, sadaka zake, mapambo zake, na hata ibada zake zote zilikuwa ni mifano ambayo iliashiria kitu ambacho kilikuwa kikuu zaidi. Maskani hayo yalikuwa ni kivuli ambacho kiliwakilisha ukweli halisi ambao ungekamilika ndani yake Kristo (Waebrania 8:5; 10:1). Katika mpangilie na ibada za Maskani hayo tunapata taswira yenye urembo mwingi wa kazi ya Mungu ya wokovu ndani ya muumini kupitia kwa Yesu Kristo, na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya muumini huyo.




### ① Maskani ya Mungu

**Maelezo Yake:** Maskani ya Mungu yaliundwa kulingana na mpango ambao Mungu alimfunulia Musa—muundo wake basi haukufuata mpango wa kibinadamu. Pale ndani kulikuwa na Mahali Patakatifu (hema ambayo ilikuwa na vyumba viwili), na pia Ua lililozunguka mahali hapo (Hesabu 3:7-8). Mahali Patakatifu palikuwa na kipimo cha dhiraa (mikono) 30 × 10 × 10 (au futi 45 × 15 × 15), na kugawanywa kwa sehemu mbili, Mahali Patakatifu, na pia Patakatifu pa Patakatifu. Ua lenyewe lilizungukwa na nguo (pazia) iliyotundikwa toka juu hadi chini (Kutoka 27:9-18). Napo Mahali Patakatifu palifunikwa kwa mapazia mengi pamoja na ngozi. Kiingilio chake kilifunguka kuelekea upande wa mashariki, kumaanisha kwamba ilimbidi mtu aukaribie uwepo wa Mungu kulingana na jinsi ambavyo Mungu Mwenyewe alichagua.

**Kusudi Lake:** Hapa palikuwa ni mahali pa Mungu kudumu kati ya wana wa Israeli, na mahali pa Mungu kukutana na mwanadamu (Kutoka 25:8, 22). Kupitia kwa muundo wake, mapambo zake, na ibada zake, Mungu alidhihirisha utakatifu wake, na pia haja ya mwanadamu kupata utakaso, pamoja na hatua za kupata wokovu. Ujenzi wa Maskani hayo ulipokamilika uwepo wa Bwana ulijaa humo ndani kwa utukufu mkuu (Kutoka 40:34). Uwepo huo ulidumu katika Maskani hayo kwa takriban miaka 480, kuanzia wakati wa wana wa Israeli Kutoka Misri, hadi wakati Sulemani alijenga hekalu.

**Ukamilifu Wake:** Kristo ndiye Maskani ya kweli (Waebrania 8:2), na ndani yake Yeye waumini wanafanyika hekalu la Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 3:16). Maskani hayo ya Mungu kwa ukamilifu wake ni jambo ambalo linaonyesha mpango wa Mungu wa wokovu kupitia kwa Kristo. Muundo wake—ambao ulikuwa na vyumba viwili maalumu—unaweza kuchukuliwa kuwa unadhihirisha kazi mbili kuu za Mungu kupitia neema: kuhesabiwa haki kwa damu ya Yesu, na pia utakaso unaotokana na kujazwa Roho Mtakatifu.

## ② Ua la Maskani (ya Mungu)




Maelezo Yake: Ua la nje lilikuwa na kipimo cha dhiraa (mikono) 100 × 50 (futi 150 ×75), na humo kulikuwa na Madhabahu ya Kuchomea Sadaka (Kutoka 27:1-8), pamoja na Birika la kuogea (Kutoka 30:18-21). Kiingilio chake katika upande wa mashariki lilikuwa ni lango la nguo ya rangi ya samawi, na rangi ya zambarau, pamoja na nyekundu (Kutoka 27:16).

Kusudi Lake: Hapa palikuwa mahali pa kutolewa sadaka na tendo la kuoga—ambayo ndio njia pekee za kuingia maskani ya Mungu. Dhambi ilihitaji kupata utakaso wa damu, ambayo ndio njia Mungu amechagua ili mwanadamu aweze kumfikia. Makuhani nao walitakiwa kuoga kabla ya kufanya huduma zao.

Ukamilifu Wake: Ua hili linawakilisha tendo la kumfikia Mungu na pia mtu kutengwa kutokana na ulimwengu. Kupitia kwa lile lango moja tu Yesu Kristo (Yohana 10:9), mtu aliyetubu hupata msamaha kupitia sadaka ya Yesu (Waebrania 9:22; Warumi 5:1)—jambo ambalo kivuli chake cha awali ni yale Madhabahu ya Kuchomea Sadaka, mahali pale ambapo damu ilimwagwa. Hapo kwenye Birika la Kuogea mtu huweza kuoshwa na kupata uzao kwa mara ya pili (Waefeso 5:26; Tito 3:5). Basi kwa njia ya kuhesabiwa haki muumini anafanyiwa maandalizi ili kuweza kuingia Mahali Patakatifu.

## ③ Mahali Patakatifu



**Maelezo Yake:** Mahali Patakatifu palikuwa na kipimo cha dhiraa (mikono) 20 × 10 × 10 (futi 30 × 15 × 15), na hapo kulikuwa na Meza ya Mikate ya Wonyesho, Kinara cha Taa cha Dhahabu, pamoja na Madhabahu ya Kufukizia Ubani (Kutoka 25:23-40; 30:1-8). Mahali hapo palikuwa pameganywa kutoka kwa Ua kwa kutumia pazia ya kwanza ya rangi ya zambarau, na rangi nyekundu, na pia kitani nzuri yenye kusokotwa (Kutoka 26:36). Ni makuhani pekee ndio waliruhusiwa kuingia humo, wakihudumu mbele zake Bwana kila siku.

**Kusudi Lake:** Mahali hapa palikuwa ni pa kufanyia ibada kila siku. Mkate ulikuwa ishara ya Mungu kukutana na mahitaji ya watu wake, nacho Kinara kiliwakilisha mwanga wake, huku ubani ukiwakilisha maombi ya watu wake. Kitani (pazia) ya kwanza iliwakumbusha wana wa Israeli kwamba ili waweze kumfikia Mungu walihitaji kutoa sadaka kwenye Madhabahu, na pia kuoga kwenye Birika la Shaba; jambo hili likitilia mkazo kwamba maisha ya kiroho huanza kwa njia ya toba na mtu kufanywa upya.

**Ukamilifu Wake:** Mahali Patakatifu panawakilisha hali ya mtu kuhesabiwa haki, yule ambaye amehuishwa kiroho na Mungu. Hapa ndipo muumini hula chakula cha kiroho kutoka kwa Kristo, aliye Mkate wa Uzima (Yohana 6:35), huku akitembea kwa mwanga wake (Yohana 8:12), na kufanya maombi ambayo yanakubalika kupitia maombezi yake Yesu (Waebrania 7:25; Ufunuo 8:3-4). Mahali Patakatifu panawakisha tendo la kuzaliwa mara ya pili na pia maisha ya ushirika wa kila siku na Mungu.

## ④ Patakatifu pa Patakatifu


**Maelezo Yake:** Chumba hiki cha ndani kilikuwa mche mraba kamili, wenye kipimo cha dhiraa (mikono) 10 × 10 × 10 (futi 15 × 15 × 15). Humo ndani kulikuwa na Sanduku la Agano, Kiti cha Rehema, na makerubi yaliyokuwa juu yake (Kutoka 25:10-22; Waebrania 9:3-5). Mahali hapa palitengwa kutoka kwa Mahali Patakatifu kwa pazia la pili, ambalo lilipambwa makerubi kwa urembo mkuu (Kutoka 26:31-33). Kuhani mkuu ndiye mtu pekee angeingia humo ndani—lakini tu katika Siku ya Upatanisho, ambayo ilisherehekewa mara moja kwa mwaka (Walawi 16:2, 14).

**Kusudi Lake:** Hapa ndipo palikuwa makazi ya Mungu ya moja kwa moja, mahali ambapo utukufu wake ulionekana kupitia makerubi. Pazia la pili liliwatenga watu wengine wote, na likawa tangazo kwamba mwanadamu mwenye dhambi hangeweza kuingia katika uwepo mtakatifu wa Mungu. Katika Siku ya Upatanisho, kuhani mkuu aliingia humo huku akiwa na damu ya kunyunyizia Kiti cha Rehema—na kwa njia hiyo kufanya utakaso kwa ajili ya wana wa Israeli, huku akibeba majina yao mbele zake Bwana (Walawi 16:17; Kutoka 28:29).

**Ukamilifu Wake:** Mahali Patakatifu pa Patakatifu panawakilisha moyo wa muumini uliojaa uwepo wa Roho Mtakatifu, mahali pale ambapo Mungu hudumu kwa ukamilifu wa neema yake (1 Wathesalonike 5:23). Hii ni ishara ya kazi ya kiwango cha pili cha neema yake—yaani utakaso kupitia kwa Roho Mtakatifu. Kwa njia ya damu ya Kristo inayotutakasa, njia ya mtu kupita na kuingia ndani ya pazia sasa imefunguliwa. Wakati Yesu alipokufa pazia “likapasuka vipande viwili” (Mathayo 27:51), na hili likawa tangazo kwamba kupitia sadaka yake waumini sasa waliweza kufika kwenye uwepo wake Mungu (Waebrania 10:19-20).

# Mapambo za Maskani

## ⑤ Madhabahu ya Sadaka za Kuchomwa




**Maelezo Yake:** Madhabahu ya Sadaka za Kuchomwa yalikuwa pale kwenye Ua, ukiingia tu langoni la Maskani ya Mungu (Kutoka 27:1-8). Madhabahu haya yaliundwa kwa mbao za mshita iliyofunikwa kwa shaba, na kipimo chake kilikuwa dhiraa (mikono) 5 × 5 × 3 (takriban futi 7.5 × 7.5 × 4.5). Vikuku vinne vya dhahabu vilitokeza katika pembe zake nne, ndani mkiwa na wavu wa shaba. Hii ilikuwa ndio samani (fenicha) iliyokuwa kubwa sana katika Maskani hayo ya Mungu, na ikawa inaonekana na kila mtu aliyeingia humo ndani.

**Kusudi Lake:** Mahali hapa ndipo kulitolewa sadaka ya dhambi. Damu iliyomwagwa hapo ilikuwa ukiri kwamba utakaso lilikuwa jambo lililohitajika (Walawi 17:11), kwa maana bila umwagaji wa damu hakuna msamaha (Waebrania 9:22). Madhabahu haya yalikuwa karibu na hapo langoni kuonyesha kwamba hakuna mtu ambaye angeweza kumkaribia Mungu bila kutolewa kwa sadaka.

**Ukamilifu Wake:** Madhabahu ya Sadaka za Kuchomwa yanamwashiria Kristo, ambaye ndiye "Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29). Kwa sadaka ile moja yake ambayo ni kamili, Yeye alitushindia ukombozi wa milele, na hakuna sadaka nyingine ambayo inahitajika sasa (Waebrania 9:26). "Tuna madhabahu" ndani yake Yesu (Waebrania 13:10), na hakuna yeyote anaweza kuwa na ushirika na Mungu bila kuanza na toba pamoja na imani katika utakaso wake (Warumi 5:9). Madhabahu ya Sadaka za Kuchomwa yanawakilisha kazi ya kwanza kuu ya neema: wokovu unaotufikia kwa njia ya toba na imani katika Kristo aliyesulubiwa.

## ⑥ Birika la Shaba

**Maelezo Yake:** Birika la shaba lilikuwa limesimamishwa kati ya Madhabahu ya Sadaka za Kuchomwa na Maskani yenyewe (Kutoka 30:17-21). Birika hilo la shaba lilikuwa limeundwa kwa kutumia vioo vya wanawake (Kutoka 38:8), na lilikuwa limejaa maji.




**Kusudi Lake:** Baada ya kutoa sadaka zao makuhani walitakiwa kuoga pale kwenye Birika la Shaba kabla ya wao kuhudumu Mahali Patakatifu. Walitakiwa kunawa mikono na miguu yao ili "ili wasife" (Kutoka 30:20-21).

**Ukamilifu Wake:** Birika hilo la shaba liliashiria haja ya mtu kujichunguza mwenyewe, kupata utakaso, na pia kuhuishwa kwa muumini (Tito 3:5) kupitia Roho na Neno la Mungu (Waefeso 5:26; Yohana 15:3). Kama vile makuhani walioga kabla ya kuingia kwenye Madhabahu ya Mungu, ndivyo muumini anahitaji kuoshwa kutokana na unajisi wote ili amtumikie Mungu kwa njia inayokubalika. "Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:7, 9).

> ***Kwa pamoja,*** *Madhabahu ya Sadaka za kuchoma na Birika la Shaba ni mambo ambayo yanaonyesha kazi mbili ambazo haziwezi kutenganishwa; kwa njia ya kuhesabiwa haki na pia kuhuishwa kwa mwanadamu—dhambi inapata kusamehewa na pia moyo unatakaswa, na kwa njia hiyo kumfanya muumini kufanywa "kiumbe kipya" ndani yake Kristo (2 Wakorintho 5:17; Warumi 8:2).*


## ⑦ Meza ya Mikate ya Wonyesho



**Maelezo Yake:** Meza hii iliundwa kwa mbao za mti wa mshita, na kufunikwa kwa dhahabu safi (Kutoka 25:23-30), na ilikuwa na kipimo cha dhiraa (mikono) 2 × 1 × 1.5 (takriban futi 3 × 1.5 × 2.25). Juu yake kulikuwa na mikate kumi na miwili, ambayo ilipangwa kwa mistari miwili, na ambayo ililiwa na Haruni na wanawe, na kubadilishwa kila siku ya Sabato.

**Kusudi Lake:** Meza hii ilikuwa ni ishara ya uwezo wa Mungu wenye kudumu wa kukutana na mahitaji ya watu wake. Mikate hiyo ambayo ilijulikana kama "Mikate ya Uwepo Wake" ilidumu mbele zake Bwana daima (Walawi 24:5-9).

**Ukamilifu Wake:** Meza hii inamwashiria Kristo, yule ambaye ndiye Mkate wa Uzima (Yohana 6:35). Kama vile makuhani waliila mikate hiyo ya wonyesho, ndivyo waumini wanavyomla Kristo kwa imani, na kwa njia hii kupata chakula cha kiroho kupitia kwa Neno lake na pia Roho wake (Mathayo 4:4). Hili ni jambo linalotufundisha kwamba ni kwa kupitia ushirika unaodumu kati ya muumini na Kristo, ambaye ndiye Mkate wa uzima unaotoka mbinguni, ndio jambo la pekee linaloweza kudumisha watu wake.




## ⑧ Kinara cha Dhahabu cha Taa (Menorah)

**Maelezo Yake:** Kinara hiki kiliundwa kwa talanta moja ya dhahabu safi (Kutoka 25:31-40), nacho kilikuwa na matawi sita kutoka hapo ubavuni mwake, na hivyo kikawa na matawi saba kwa jumla. Kwa kawaida kinara hiki kilikuwa na urefu wa futi tano, na kiliundwa kwa mfano wa maua ya mlozi, tovu na ua lake.

**Kusudi Lake:** Kinara hiki cha taa kilikuwa kimewekwa Mahali Patakatifu, kando ya Meza ya Mikate ya Wonyesho, na ndicho pekee kilileta mwangaza hapo ndani ya Mahali Patakatifu (Kutoka 27:2021). Taa hizi ziliwaka bila kukoma, na kupata nishati kutoka kwa mafuta yaliyoletwa na wana wa Israeli, huku kikitunzwa na makuhani toka jioni hadi asubuhi.

**Ukamilifu Wake:** Kinara hiki cha taa kinamwakilisha Kristo, ambaye ndiye Mwanga wa Ulimwengu (Yohana 8:12). Waumini hawana nuru yao ya kibinafsi; nuru ya kweli hupatikana kutoka kwa Kristo kupitia kwa mafuta ya Roho (2 Wakorintho 4:6). Nao Wakristo wameitwa ili waangaze nuru ya Yesu katika ulimwengu huu wenye giza (Mathayo 5:14-16); kwa maana Yeye ndiye hutoa mwangaza kwa kanisa lake (Ufunuo 1:20).

## ⑨ Madhabahu ya Kufukiza Ubani (Madhabahu ya Dhahabu)




**Maelezo Yake:** Madhabahu haya ya Dhahabu yaliundwa kwa mbao za mti wa mshita na kufunikwa kwa dhahabu safi (Kutoka 30:1-10). Kipimo chake kilikuwa dhiraa (mikono) 1 × 1 × 2 (takriban futi 1.5 × 1.5 × 3). Madhabahu haya yalikuwa yametengenezwa hapo mahali kabla ya mtu kufikia pazia lile, mbele ya mahali Patakatifu pa Patakatifu. Nao ubani ulifukizwa hapo kila asubuhi na kila jioni.

**Kusudi Lake:** Wakati ubani huo ulikuwa ukipaa juu, hii ilikuwa ni ishara ya maombi ya watu wa Mungu, wakati yakikwea 'juu' ili kumfikia Mungu (Zaburi 141:2). Kwa sababu ulifukizwa kwa kutumia moto mtakatifu kutoka kwa Madhabahu ya Sadaka za Kuchomwa, tendo hili lilikuwa ni ukiri kwamba maombi hayana budi kuandamana na sadaka. Damu ya matoleo ya aina fulani ya dhambi ilipakwa kwenye pembe za madhabahu hayo (Walawai 4:7, 18), jambo ambalo liliwakumbusha wana wa Israeli kwamba hata mahali pa maombi palihitaji kusafishwa kwa njia ya tendo la upatanisho. Na katika Siku ya Upatanisho, damu hiyo ilipakwa kwenye pembe baada ya kuhani mkuu kuingia Patakatifu pa Patakatifu (Walawi 16:18). Kwa sababu yalikuwa yamesimamishwa hapo kabla ya mtu kufikia pazia lililokuwa mbele ya Sanduku la Agano, Madhabahu hayo ya Kufukiza Ubani yalikuwa daima ni ukumbusho kwamba maombi na ibada ndio njia ambayo Mungu amechagua ili wanadamu waweze kumfikia.

**Ukamilifu Wake:** Madhabahu ya Dhahabu yaliangazia maombi na sala (Ufunuo 8:3-4). Kristo, ambaye ndiye Kuhani Mkuu wetu na ambaye "yu hai sikuzote ili atwombee;" kupitia kwake maombi ya watakatifu yanapaa 'juu' na kukubalika mbele zake Mungu. Damu iliyopakwa kwenye pembe ilikuwa ishara ya awali kwamba ni kwa njia ya sadaka ya Kristo ndipo ibada inatakaswa na kukubalika. Na kwa anayemuamini Kristo, Madhabahu hayo ni ishara ya maisha ya maombi na ushirika na Baba, ushirika ambao unatokana na moyo uliotolewa mhanga kwake Mungu (Warumi 12:1).


### ⑩ Sanduku la Agano



**Maelezo Yake:** Sanduku la Agano lilikuwa limeundwa kwa mbao za mti wa mshita na kufunikwa kwa dhahabu safi (Kutoka 25:10-22). Kipimo chake kilikuwa dhiraa (mikono) 2.5 × 1.5 × 1.5 (takriban futi 3.75 × 2.25 × 2.25). Ndani yake kulikuwa na mbao za mawe ambazo ndani mwake mliandikwa Sheria ya Musa, na pia kopo la dhahabu lililokuwa na mana, pamoja na ile fimbo ya Haruni iliyochipuka (Waebrania 9:4). Vikuku viliwekwa ndani ya Sanduku hilo kwa ajili ya kulibeba, kwa maana kamwe halikutakiwa kuguzwa na mtu yeyote kwa njia ya moja kwa moja.

**Kusudi Lake:** Sanduku la Agano lilikuwa ndicho kitu kilikuwa kitakatifu zaidi katika Maskani hayo ya Mungu. Sanduku lenyewe lilikuwa ndicho kitovu cha agano kati ya Mungu na wana wa Israeli. Pia lilihifadhi ushahidi kwamba Mungu hukutana na mahitaji ya watu wake, na pia sheria yake Mungu, pamoja na ukuhani wenyewe — mambo ambayo ndio yalikuwa ishara ya uhusiano wa kudumu kati ya Mungu na watu wake. Mahali popote ambapo Sanduku hilo lilikuwa, kulikuwa pia na utukufu dhahiri wa uwepo wake Mungu.

**Ukamilifu Wake:** Sanduku hili la  Agano linamwashiria Kristo kwa njia ya moja kwa moja. Ndani yake Kristo Sheria ilitimizwa kwa ukamilifu kabisa (Mathayo 5:17). Yeye ndiye Mkate wa kweli toka mbinguni (Yohana 6:51); na pia Yeye ndiye Kuhani Mkuu wa milele mwenye ukuhani usiobadilika (Waebrana 7:24). Kila chote kilichokuwa kwenye Sanduku hilo kinapata uhalisi wake ndani yake Yesu. Katika Agano Jipya Sanduku hilo la Agano linawakilisha Kristo akiwa ndani yetu—ijapokuwa Yeye sasa hadumu katika sanduku kama hilo la kale, bali katika mioyo ya muumini aliyetakaswa.



### ⑪ Kiti cha Rehema na Makerubi

**Maelezo Yake:** Kiti cha Rehema kiliundwa kutokana na dhahabu safi, na kilikuwa kama kifuniko cha Sanduku la Agano (Kutoka 25:17-22). Kipimo chake kilikuwa dhiraa (mikono)  2.5 × 1.5 (takriban futi 3.75 × 2.25). Makerubi wawili wa dhahabu walikifunika kiti hicho, huku mabawa yao yakiwa yameinuliwa juu yake, na wao wakawa wametazamana kwa kuelekea Kiti hicho cha Rehema.

**Kusudi Lake:** Kiti hiki ndicho kililikuwa kama jukwaa la uwepo wake Mungu katika nchi ya Israeli. Katika Siku ya Upatanisho, kuhani mkuu alinyunyizia damu juu yake ili kuwapatanisha watu na Mungu wao (Walawi 16:14-15). Juu ya Kiti cha Rehema, katikati mwa makerubi hao wawili, Mungu alidhihirisha uwepo wake na kunena naye Musa—huku sauti yake ikitoka mahali Patakatifu pa Patakatifu, hata ingawa wakati huo Musa alikuwa amekaa nje ya pazia hilo (Kutoka 25:22: Hesabu 7:89).

**Ukamilifu Wake:** Ukamilifu wa Kiti cha Rehema unapatikana ndani ya Kristo, ambaye ndiye Kipatanisho chetu (Warumi 3:25; 1 Yohana 2:2). Makerubi hao nao hutilia mkazo umuhimu wa utakatifu na ukuu wa uwepo wa Mungu; mahali ambapo ndipo hukumu za kiungu na rehema zake hupatana na sadaka yake Kristo. Katika Agano Jipya, muumini aliyetakaswa hufanyika makazi ya Mungu—na mahali ndipo rehema na utukufu hudumu—ila sio utukufu wa dhahabu, bali ni ule unaotokana na moyo uliofanywa mtakatifu na Roho wake Mungu (1 Wakorintho 3:16; 2 Wakorintho 6:16). Kutokana na kazi ya utakaso wa Kristo, na kupitia Roho wake anayedumu ndani yetu, sasa mawasiliano ya kudumu kati ya mwanadamu na Mungu ni jambo ambalo linawezekana.

**"Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli,**
**baada ya siku zile, asema BWANA;**
**Nitatia sheria yangu ndani yao,**
**na katika mioyo yao nitaiandika;**
**nami nitakuwa Mungu wao,**
**nao watakuwa watu wangu."**

**Yeremia 31:33**